# Utekelezaji wa Sera za Elimu na Afya

## Programu ya Kuboresha Serikali za Mitaa imeleta mabadiliko?




actionaid

# Utangulizi

Historia ya Maboresho ya Serikali za Mitaa inaanzia tangu enzi za ukoloni. Kwa sasa imefupishwa na inapatikana kwenye Sera ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1998. Sera hii inaelezea kwa kina dhamira ya serikali kuhusu mfumo wa Serikali za Mitaa zilizoboreshwa. Malengo ya jumla ya sera hii ni kuboresha upatikanaji wa huduma kwa jamii, mkakati mkuu ukiwa kuhamisha madaraka ya kuongoza na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa Serikali za Mitaa kutoka serikali kuu. Programu ya Kuboresha Serikali za Mitaa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ndicho chombo maalum kinachoshughulikia maboresho hayo.

Chapisho hili rahisi ni juhudi za makusudi za ActionAid International Tanzania kuweza kuwasilisha kwa wananchi walio wengi matokeo ya utafiti kuhusu Programu ya kuboresha Serikali za Mitaa na namna inavyotoa huduma kwa wananchi hasa kwenye sekta z a Elimu na Afya. Utafiti huu ulifanyika kwenye wilaya za Mkuranga, Liwale, Tandahimba na Kigoma. Utafiti ulizingatia vipengele vikuu vitatu ambavyo ni Utawala, Fedha na Usimamizi wa Fedha na Upatikanaji wa Huduma.

Lengo kuu la utafiti huo likiwa ni kutia chachu Programu ya Kuboresha Serikali za Mitaa kwenye wilaya zilizoorodheshwa hapo juu.

# Wananchi wanashiriki vipi?




Kulingana na maoni ya wananchi waliohojiwa kwenye wilaya hizo nne , kiwango cha uongozi wa serikali za mitaa hakiridhishi. Kuthibitisha hilo, asilimia 72 ya wananchi walioshiriki kwenye utafiti huo walikuwa na mtazamo kuwa viongozi wa serikali za mitaa wa maeneo yao wameshindwa kukabili kero sugu zinazowasumbua wananchi wala kuzingatia matakwa yao. Pia asilimia 79 hawakuwa na taarifa ya kuwepo kwa programu hii na asilimia 80 wamesema viongozi hawafanyi kazi zao kwa uwazi. Dalili pekee zilizoonyesha utendaji mzuri ni kujitokeza na kushiriki kwa wananchi kwenye mikutano ya kamati za shule na zile za vijiji ambayo ilihudhuriwa na zaidi ya asilimia 70 ya wananchi waliohojiwa. Hata hivyo, takwimu hizo hapo juu zinatoa tafsiri kwamba wananchi hawajafafanuliwa kuwa ushiriki wao ni sehemu ya maboresho kwa sababu hata maboresho yenyewe wengi wao hawayajui. Ukweli huu uko kinyume na jinsi serikali inavyoamini kuwa kuna ongezeko kubwa la uelewa wa jamii kuhusu Programu hii ya Maboresho ya Serikali za Mitaa.

# Kuna uwazi na ushirikishwaji?

Taarifa za uhakika kutoka kwa wananchi wenyewe zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 80 ya wananchi waliohojiwa hawakuwa na uelewa kuhusu mabadiliko ya mfumo wa mgawanyo wa kodi, ushuru na mapato mengine kwenye serikali za mitaa na pia hawana uwezo wa kuhoji chochote kuhusu taarifa zinazohusu makusanyo ya kodi na ushuru unaokusanywa wala hawapewi fursa ya kutoa maoni yao kwenye mipango ya kodi na ushuru unaokusanywa kutoka vijijini mwao.






# Viongozi wanamudu vema usimamizi wa fedha?

Wananchi wengi waliohojiwa kuhusu uwezo wa viongozi wa ngazi za chini katika kusimamia viwango vikubwa vya fedha walionyesha kutoridhika. Asilimia 56 ya waliohojiwa walidai viongozi wa vijiji walio wengi hawana uwezo wa kusimamia viwango vikubwa vya fedha kutokana na kutokuwa na elimu ya usimamizi wa fedha. Pia wamelalamikia uhaba wa vitendea kazi vijijini na ulinzi madhubuti.




# Nani asimamie fedha za maendeleo ya wananchi?

Wananchi wameonyesha kukosa imani kwa mtu yeyote linapokuja suala la usimamizi wa fedha ili kupata huduma kwa ubora zaidi. Asilimia 41 wameonyesha kuwa kwa upande wao hata angepewa mtu yeyote nafasi hiyo ya kusimamia fedha haitokuwepo nafuu yoyote.

# Mabadiliko katika upatikanaji wa huduma yanaonekana?




Maboresho yamelenga katika kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii. Kwa ujumla, wananchi waliohojiwa kwenye wilaya zilizofanyiwa utafiti wameonyesha kuridhishwa hasa kwa upande wa huduma ya Elimu kuliko Afya.




# Gharama za huduma zitolewazo zinaridhisha?

Maboresho kwenye Serikali za Mitaa yamelenga pia kuhakikisha kuwa huduma za jamii zinapatikana kwa gharama nafuu. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa gharama za huduma za afya na elimu ni nzuri. Hii ndio sababu asilimia 87 ya waliohojiwa wamesema kuwa gharama za huduma ya afya zinaridhisha wakati asilimia 90 wamesema vivyo hivyo kwa upande wa huduma za elimu.




# Nini kifanyike katika utekelezaji?

Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ingeshirikiana na asasi za kijamii ili kubuni njia sahihi za kufanya maboresho ya serikali za mitaa na sera vinaeleweka vema kwa wananchi ili waweze kutambua lengo la programu hii. Kwa kufanya hivyo, wananchi wataweza kushiriki vilivyo katika utekelezaji wa programu hii na sera zinasemaje ili hatimaye kuweza kudai yale wanayopaswa kutendewa na viongozi wa serikali za mitaa.

# Mazingira ya kazi kwa watendaji yaboreshwe vipi?

Uhaba wa watendaji kwenye taasisi nyingi zinazohusika na utoaji wa huduma hizo unaweza kupunguzwa endapo serikali itaanzisha na kutekeleza mikakati madhubuti yenye kuweka mazingira mazuri kwa watendaji hasa kwenye wilaya masikini zaidi nchini. Posho nzuri na marupurupu mengine vyaweza kuwa miongoni mwa mikakati inayoweza kutumika kuvutia watendaji ili waweze kwenda kufanya kazi kwenye maeneo hayo duni.



# Wadau wa maendeleo ya Elimu na Afya wafanye nini?

Wadau wa maendeleo ya elimu na huduma za afya wanapaswa kuingilia kati katika kuboresha miundombinu ya maendeleo ya ubora wa elimu na huduma za afya. Kwa mfano, hivi sasa madarasa yanajengwa kwa wingi sehemu mbalimbali nchini lakini hakuna maktaba mashuleni!




Kwa kuwa uongozi wa vijiji haujajiandaa vema kubeba jukumu la usimamizi wa fedha., ipo haja ya kuviwezesha vijiji viweze kupokea jukumu hilo la kusimamia fedha nyingi kwa kuwapa mafunzo maalum watendaji wao kwa maendeleo ya vijiji vyao.

# ActionAid International Tanzania ni nini?

ActionAid International Tanzania ni mojawapo ya matawi ya ActionAid International ikiwa na dira ya jamii ya Kitanzania ambayo kila mwanajamii hana umasikini na anapata haki na kuheshimiwa utu wake. Lengo la ActionAid International Tanzania ni kutokomeza umasikini kwa kuwawezesha walio masikini, waliosahaulika au kubaguliwa pia taasisi za kijamii waweze kushirikishwa kwa kutumia mbinu zinazozingatia haki (Rights Based Approach).

Ikiwa imeanzishwa mwaka 1998, ActionAid International Tanzania imekuwa ikiimarisha jitihada zake za kukabiliana na umasikini kwenye wilaya masikini zaidi nchini ambazo ni Liwale na Kilwa(Lindi), Tandahimba na Newala (Mtwara), Kigoma Vijijini(Kigoma), Mkuranga, Mafia na Bagamoyo (Pwani), Unguja na Pemba(Zanzibar),Singida Vijijini na Chamwino (Dodoma).

End Poverty. Together. End Poverty. Together.

Kimetolewa na
ActionAid International Tanzania
Kitalu 96, Mikocheni Eneo la Viwanda,
Ghorofa ya 2, Jengo la CT,
S.L.P. 21496
Dar-es-Salaam,
Tanzania.